# WAKATI UJAO...UKWELI KUHUSU WAKATI UJAO...UKWELI




**MAMBO HAYA YANATUHUSU SISI WOTE! JE, UNGELIPENDA KUJUA NI NINI KITAKACHO FUATA? BASI ENDELEA KUSOMA!**

## MAMBO YAJAYO KWA UWAZI

Kwa miaka michache iliyopita, dunia imenshuhudia tukio moja baada ya lingine. Ukame, mafuriko, vimbunga vya kuharibu, mitetemeko ya ardhi, yote yamefanyika yakifuatana kwa karibu sana. Maelfu walipoteza maisha yao katika ajali mbali kwenye nchi kavu, majini na hewani; ilhali wengine mamilioni wakifa njaa, mataifa mengi yamefilisika, wasiweze kulipa madeni yao. Vita, migomo, mpasuko wa idadi ya watu duniani, kuharibiwa kwa mazingira, yanamfanya mwanadamu kuutazama wakati ujao kwa uoga mno.

**Mengi ya matukio haya yametabiriwa katika Biblia** (Math. 24:4-31, Lk. 21:25-28, Ufunuo 6:12-17, 16, 17, 18). **Kila wakati, Mungu ameionya dunia kuhusu hukumu ijao kwa sababu ya uasi wetu** (Isaya 24:5-20, 46:9-10, Am. 3:7, Ufunuo 1:1).


## FUNZO KUTOKA MATUKIO YA ZAMANI

Kwa mfano, Mungu alimuonya Nuhu kuhusu **mafuriko**, Abraham na Lutu kuhusu **uharibifu wa Sodoma na Gomora** na Musa kuhusu **mapigo ya Misri**.

Matukio haya yameandikwa kutuonya sisi ili tupate kuelewa ya kwamba unabii wa Biblia umetimia au utatimia (1 Wakor. 10:6-12, 2 Petro 2:5-9, Waebrania 4:11).

Kwa hivyo, tunapata onyo la Mungu kwa kizazi cha mwisho jinsi unayowakilishwa katika

**UJUMBE WA MALAIKA WATATU**



ambao tunaupata katika Ufunuo 14 jinsi alivyoandika Yohana. Huu ni mwito wa mwisho kwa watu wote ambao unatolewa na Mungu kabla ya kurudi kwa Kristo kama Mfalme na Hakimu.

Ujumbe huu unalo onyo la muhimu sana kuhusu hukumu katika Biblia:

**(1)** ***"Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja.*** *Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na chemchemi za maji."*

**(2)** *"Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo wa ghadhabu ya uasherati wake."*

**(3)** *"Mtu awaye yote* ***akimsujudu huyo mnyama*** *na* ***sanamu yake****, na* ***kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake****, yeye naye atakunywa katika mvinyo wa ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele za malaika watakatifu na mbele za Mwana-Kondoo. Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana na usiku, hao wamsujuduo huyo* ***mnyama*** *na* ***sanamu yake****, na kila aipokeaye* ***chapa ya jina lake****"* **Ufunuo 14:6-11.**

Onyo hili ni la muhimu sana kwa kila mtu! Lakini tutaepukaje kumsujudu *mnyama* na *sanamu yake* au kuipokea *chapa yake* ikiwa hatujui ni nini maana ya mnyama na sanamu yake? Kukosa ufahamu katika jambo hili kuna matokeo ya kifo. *„Watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa"* Hos. 4:5 (Isaya 29:13-14).

Hata hivyo, Mungu ameahidi hekima kwa wenye haki (Meth. 2:1-7, Dan. 12:4,10, Math. 7:7-8).

*"Kama mimi niishivyo, asema Bwana Mungu, sikufurahii kufa kwake mtu muovu; aghairi mtu muovu, na kuiacha njia yake mbaya, akaishi. Ghairini, ghairini, mkaache njia zenu mbaya; mbona mnataka kufa, Enyi nyumba ya Israeli?"* Ez. 33:11 (Linganisha 2 Petro 3:10-11, Mal. 3:18, 4:1-2).

## Ni nini maana ya mnyama na alama yake?

Kabla ya kumjadili mnyama, lazima tuelewe historia iliyomtangulia huyu mnyama. Pahali pazuri pa kuanzia ni katika kitabu cha Daniel, ambacho kinashughulikia unabii, kuanzia karne ya sita kabla hajazaliwa Yesu hadi wakati wa leo.


**Kutafsiri mfano katika Biblia hautegemei ujuzi wa mtu. Unabii ni historia iliyoandikwa kabla yake kutendeka. Biblia yenyewe inatupatia mwelekeo na ufahamu** (2 Pet. 1:20).




Mnyama katika unabii anawakilisha mfalme au ufalme. Jambo hili ni dhahiri katika Dan. 7:17,23: *"Wanyama hao wakubwa walio wanne ni wafalme wanne watakaotokea duniani... Huyo mnyama atakuwa wa nne juu ya dunia."*

Katika Dan. 7:3 imeandikwa: *"Ndipo wanyama wakubwa wanne wakatoka baharini..."* **"Bahari"** au **"maji"** huwakilisha *„jamaa na makutano na mataifa na lugha."* Ufunuo 17:15 (Isaya 8:7).

Katika Dan. 7 nabii anaziona falme za dunia zikiwakilishwa na **"Wanyama"** Maelezo sawa na hayo tunayapata katika Dan. 2:27-45 ambapo kila kiungo kinaeleza mwelekeo wa mwanadamu katika siku za usoni.




## SIMBA

*"Wa kwanza alikuwa kama simba..."* Dan. 7:4 (Dan. 2:37-38). Simba anawakilisha ufalme wa **Babeli uliotawala dunia miaka ya** 608-538 kabla Yesu kuzaliwa, utawala wa pekee siku za Danieli. Sanamu ya Simba mwenye mabawa imehifadhiwa katika jumba la hifadhi la Pergamon mjini Berlin, Ujerumani.



## DUBU

*"Na tazama, mnyama mwingine, kama dubu, naye aliinuliwa upande mmoja, na mifupa mitatu ya mbavu ilikuwamo kinywani mwake katika meno yake; wakamwambia mnyama huyu hivi; inuka ule nyama tele."* Dan. 7:5. Mnyama huyu ni sawa na maelezo ya mikono na kifua cha shaba cha Dan. 2:32,39. Mnyama huyu anawakilisha **falme mbili za waamedi na waajemi** waliotawala baada ya Babeli miaka ya 538-331 kabla ya kuzaliwa Yesu. Waamedi ndio waliotangulia kutawala kisha badaaye Waajemi. Mikono miwili katika Dan. 2 na kuinuliwa upande mmoja katika Dan. 7, ni maelezo yanayotilia mkazo unabii huu. Upande mmoja ulikuwa na nguvu kuliko mwingine. Mbavu tatu zinawakilisha mataifa matatu ya Babeli, Lydia na Misri yaliyopigwa na Waamedi na Waajemi.



## CHUI

*"Kisha nikatazama, na kumbe! Mnyama mwingine, kama Chui, naye juu ya mgongo wake alikuwa na mabawa manne kama ya ndege; mnyama huyo alikuwa na vichwa vinne; akapewa mamlaka."* Dan. 7:6. Mnyama huyu ni sawa na yule wa Dan. 2:32,39. Ulikuwa **ufalme wa Wayunani** ukiongozwa na Alexander uliowaangusha Waajemi na kutawala miaka ya 331-168 kabla ya Yesu kuzaliwa. Alexander alipokufa, ufalme wake uligawanyika katika sehemu nne (Falme za Diadoki) zinazowakilishwa na vichwa vinne. Sehemu hizi zilikuwa Macedonia, Thrace, Syria na Misri.



## MNYAMA WA NNE

*"Baadaye nikaona katika njozi ya usiku, na tazama, mnyama wa nne, mwenye kutisha, mwenye nguvu, mwenye uwezo mwingi, naye alikuwa na meno ya chuma, makubwa sana; alikula na kuvunja vipande vipande, na kuyakanyaga mabaki kwa miguu yake; na umbo lake lilikuwa mbali kabisa na wale wa kwanza,* ***naye alikuwa na pembe kumi****"* Dan. 7:7. Mnyama huyu ni sawa na yule wa Dan. 2:33,40,41. Ufalme huu wa nne uliokuja baada wa ule wa waunani ni **ufalme wa Rumi** uliotawala kuanzia mwaka wa 168 kabla ya kuzaliwa Yesu, hadi 476 baada ya kuzaliwa. Mnyama huyu alikuwa tofauti sana na wale waliomtangulia hivi kwamba Danieli alishindwa kueleza mfano wake. Katika ufalme huo wataondoka ***"wafalme kumi"*** ni katika Dan. 7:24 inawakilisha *"wafalme kumi watakaotokea katika ufalme huu"*. Historia inaweka wazi kwamba ufalme wa Rumi uliangushwa mwaka wa **476 baada ya kuzaliwa Yesu**, na uligawanyika katika falme kumi ambazo ni mataifa kumi ya Uropa ya leo. Falme hizi kumi za Dan. 7:7 ni sawa na vidole kumi vya Dan. 2:42-44. Mataifa haya ni: (1) Ujerumani, (2) Ufaransa, (3) Uingereza, (4) Uswizi, (5) Uispania, (6) Ureno, (7) Utaliano; (8) Heruli, (9) Vandals, (10) Ostrogoths.



## PEMBE NDOGO

*"Nikaziangalia sana pembe zake, na tazama,* ***pembe nyingine ikazuka kati yao****, nayo ilikuwa ndogo, ambayo mbele yake pembe* ***tatu*** *katika zile za kwanza zikang'olewa kabisa; na tazama, katika pembe hiyo mlikuwa na macho kama ya mwanadamu, na kinywa kilichokuwa kikinena maneno makuu."* Dan. 7:8



### Alama tofauti za kutambua pembe ndogo:

**1.** Alizuka *kati* ya zile pembe (falme) kumi, na wakati alipoinuka kutawala, pembe *tatu* zilingolewa na akachukua nafasi yao.


**2.** Katika Dan. 7:24 tunaambiwa pembe ndogo inazuka *baada* ya zile kumi.

Katika historia yote ni ufalme mmoja tu unaotimiza masharti haya katika Rumi yenyewe mwaka wa **476 baada ya kuzaliwa Yesu**, Upapa, serikali ilioongozwa na mtu mmoja chini ya kanisa katoliki; ulisimamishwa. Katika kuinuliwa kwake, falme *tatu* za *Haruli*, *Vandals* na *Ostrogoths* ***"ziliangushwa"***. Kwa amri ya Justinian (Codex Justinianus), mfalme wa Rumi ya mashariki, katika mwaka wa **533 baada ya kuzaliwa kwake Yesu**. Askofu wa Roma alifanywa kuwa kiongozi wa makanisa yote ya ukristo (Ostrogoths) ndiyo waliokuwa wapingamizi wa mwisho kung'olewa kabisa mwaka wa **538** na kufukuzwa kutoka Rumi na Jemerali Balisarius. Mwaka huo ndipo Rumi ya upapa ilidhibitishwa kuwa serikali **kwa wakati uliotabiriwa** (angalia maelezo baadaye).

**3.** Katika Dan. 7:25 tunasoma *"naye atawadhoofisha watakatifu wake Aliye juu"*, maana yake ni mateso makubwa ya wakristo. Yeyote aliye na ufahamu katika historia, atafahamu ya kwamba maelezo haya yanaulenga Upapa. Mateso makali dhidi ya wakristo wakati wa zama za giza (Kuwahoji watu kuhusu imani yao, kuwachoma wazushi, vita vya kidini) haya yote yanajulikana na yamo katika kurasa za historia.



**4.** Tunazidi kusoma: *"ataazimu kubadili majira na sheria..."* Ni dhahiri ya kwamba Upapa umebadilisha amri kumi za Mungu. Katika Katakisimu ya Katoliki, utawala wa Upapa umebadilisha **sheria ya pili** *inayopiga marufuku uabudu sanamu*. Pia, Upapa umebadilisha **sheria ya nne**, *ya utunzaji wa Sabato*, iliyo sheria ya pekee kuhusu ***"Wakati"***, kwa kuifanya Jumapili siku ya kwanza ya juma, kuwa siku ya kupumzika badala ya siku ya saba ya juma (2 Wathes. 2:3-4, Zab. 94:20).




Vichwa 7 ni milima 7 inayozingira (Rumi)
Ufunuo 17:9

Walibadilisha ***"wakati"*** wa kuabudu. Wakaanzisha siku ya kuabudu isiyo ya kweli; badala ya siku ya **Saba ya juma**, Sabato isiyobadilika tangu mwanzo (Kut. 20:8-11; 31:13,16-17, Eze. 20:12, Isaya 56:2-3,6-7; Zab. 89:35, Waeb. 4:1-11, Yak. 2:10), ilyotunzwa na Kristo pamoja na Mitume (Lk. 4:16, Math. 24:20, Matendo 13:42, Waeb. 4:10-11). **Siku ya kwanza** ya juma (siku ya Jua), siku ya kuabudu jua, ikaanzishwa, kinyume kabisa na amri ya Mungu. Mungu tayari alikuwa amewaonya watu wake wasije wakaikubali hii siku bandia ya ibaada (Ufunuo 14:9-11, 16:2, 19:20, angalia Eze. 8:16-18).

**5.** *"Naye akapewa kinywa cha kunena maneno makuu ya makufuru. Akafunua kinywa chake amtukane Mungu, na kulitukana Jina Lake, na maskani yake, nao wakaao mbinguni."* Ufunuo 13:5-6, Dan. 7:8,25, Dan. 8:25, 2 Wathes. 2:3-4. Je, makufuru yanatafsiriwa vipi katika Biblia? Wakati mmoja Kristo akitafutiwa makosa, wayahudi walisema ya kwamba amekufuru, *"kwa sababu wewe uliye mwanadamu **wajifanya u Mungu**"* Yoh. 10:33. Aina nyingine ya makufuru Lk. 5:21: *"Ni nani awezaye **kusamehe dhambi** isipokuwa Mungu pekee yake?"* Aina haya ya makufuru mawili yanalenga upapa (***"Hapa duniani tunashikilia nafasi ya Mungu Mwenyezi"***, Encyc. Papa Leo wa kumi na tatu tarehe, 20-6-1894). Mara kwa mara papa huitwa "Baba Mtakatifu" hata ingawa Yesu alisema mtu yeyote asiitwe jina hili (Math. 23:9). Kwa sababu jina hili ni la Baba yetu aliye juu mbinguni pekee yake. Yoh. 17:11.

**6.** Katika Dan. 7:25, 12:7 na Ufunuo 12:14, kutawala kwa upapa kunatafsiriwa kuwa ***nyakati tatu na nusu wakati***, Ufunuo 11:2, 13:5 kama ***miezi arobaini na miwili*** Ufunuo 11:3, 12:6 kama siku ***elfu na mia mbili na sitini***.




Tafsiri ya Biblia inayoeleza ***siku moja = mwaka mmoja*** (Eze. 4:6, Hes. 14:34) ni dhahiri ya kwamba mafungu haya yote yanamaanisha miaka 1260. Wakati mmoja ni sawa na mwaka mmoja. Nyakati za zamani walihesabu mwaka mmoja kuwa siku 360. Mwezi mmoja unazo siku thelathini (Mwanzo 7:11,24, Mwanzo 8:4), kuna siku 150 ambazo ni sawa na miezi 3 ½ x miezi 12 = miezi 42, na miezi 42 x siku 30 = siku 1260, au miaka halisi 1260 katika historia.

Tunafahamu kwamba muda uliyotabiriwa ulitimizwa kwa usahihi katika historia ya upapa. Kuharibiwa kabisa kwa Ostrogoths mashariki mwa ufalme wa kirumi mwaka wa **538 baada ya kuzaliwa kwa Yesu** (ambao waliokuwa wa mwisho kupinga utawala wa Kirumi), unaeleweka kuwa ndio mwanzo wa utawala wa Upapa. Tukianza kuhesabu miaka 1260 kwanzia 538, tunafika mwaka wa **1798**. Katika mwaka huu, Pope Pius wa sita alichukuliwa mateka na mfaranza Jenerali Berthier baada ya vita vikuu vya Ufaransa. Ukatimia unabii wa: *"Mtu akichukua mateka, atachukuliwa mateka"* Ufunuo 13:10. Tangu mwaka huo, upapa haujawahi kupata nguvu sawa na zile za awali. Katiba ya kidemokrasia iliwekwa, na Rumi ikawa nchi huru, nguvu za kisiasa za Rumi zikafika mwisho, ikatimia miaka 1260 sawa na ilivyotabiriwa katika Biblia.

Katika Ufunuo 13:1-10 historia inaeleza jinsi nguvu za Upapa zilipoanza kutoka katika ufalme wa Rumi ya kishenzi, jinzi ulivyotawala miaka 1260, na jinzi ulivyopata jeraha la mauti.

**7.** Katika Ufunuo 13:3 tunasoma: *"Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti, **na pigo lake la mauti likapona. Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule.**"* Hii ni dhahiri kwamba utawala huu utakuwepo hadi Kristo atakaporudi (Tazama Dan. 7:21-22).

**8.** Wakati wa jeraha la mauti na kurejeshewa nguvu zake, mnyama mwingine anatokea: *"Kisha nikaona **mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi**; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa Mwana-Kondoo, akanena kama joka. Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake. Naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona."* Ufunuo 13:11-12.



Je, ni utawala upi unaoelezwa?

| **Mfano:** | **Maana:** |
|---|---|
| **1.** Ainuka kutoka katika Nchi (Ufunuo 13:11). | **1.** Ainuka kutoka katika nchi mpya isiyo na watu wengi. |
| **2.** Ainuka wakati ambapo Mnyama wa baharini anaanguka (1798, Ufunuo 13:1,3,10). | **2.** Ainuka kama taifa wakati wa kuanguka kwa upapa (1763-1800). |
| **3.** Ana pembe mbili kama Mwana-Kondoo (Ufunuo 13:11). | **3.** Apata nguvu zake katika misingi miwili ya tabia za Ukristo (Uhuru wa Kidini na wa kisiasa). |
| **4.** Hana taji kwenye Pembe zake (Ufunuo 13:11). | **4.** Siyo Ufalme – Aina ya taifa lilolo huru. |
| **5.** Anazo nguvu sawa na Mnyama wa kwanza (Ufu. 13:12). | **5.** Anazo nguvu kuliko mataifa yote duniani. |

Ni taifa moja duniani linalotimiza masharti haya – Marekani – mataifa mbali mbali yalishikana na kuwa taifa moja miaka ya 1763-1800. Katika **Ufunuo 13:11-18**, anaanza akiwa mpole lakini anamalizia kutawala dunia yote. **Imetabiriwa kwamba Marekani *itamfanyia mnyama sanamu* ambayo itawafanya wanadamu wote *Kumsujudia yule mnyama ambaye jeraha lake lilipona*. Sanamu hii ni sawa na utawala wa upapa kwa miaka 1260.** Maelezo ya ibaada hii yanaonyesha utawala wa kidini na kisiasa unaoshirikiana.

Katika Dan. 3:5,10,14,18,28 tunajifunza kuwa ibaada ya sanamu za watu na aina zingine sawa na hizo, ni kuabudu sanamu kinyume na amri ya Pili (Kut. 20:4-6). Ibaada ya Jumapili ni ishara ya nguvu, alama ya mamlaka ya upapa, kujiwekea sheria zao wenyewe (**wao wenyewe wanakiri ya kuwa sheria hizi ni zao wala si za Mungu!**). Unabii unaeleza kwamba Marikani itaweka sheria ya kuabudu Jumapili, (*"alama ya mnyama"*) kwa kusimamisha ***"sanamu"***. **Sanamu hii ni Uprotestanti ulioasi, mkusanyiko wa makanisa, utakaoshirikiana na serikali kuweka sheria za kidini.** Dunia yote tayari inatambua kuwa Jumapili ndio siku ya kupumzika (soma kitabu kiitwacho **Vita Kuu - "The Great Controversy"**). Ni ujeuri wa Upapa kudhani ya kuwa wanaweza kubadilisha sheria kumi, amri za Mungu. Hili ndilo litakalo kuwa swala la muhimu hivi karibuni, uamuzi wa kufa na kupona (Ufunuo 13:14-15): Kumtii Mungu au amri za watu (Mal. 3:18, 4:1, Ufunuo 16:2).

Ufahamu ya kuwa wakati huu, Marekani itafanya *"ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu"* (Wazia bomu ya mwaka wa 1945 ya Hiroshima, makombora ya hewani ya Iraq, au mwamusho wa kiroho ulio na mwanzo wake kule Marekani.) *"...Naye awakoshesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kufanya mbele ya huyo mnyama."* (soma pia Math. 24:24) *"...akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama,* (Upapa) *aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi"* Ufunuo 13:13-14. **Upapa unadai kwamba tendo la kuibadilisha Sabato hadi siku ya kwanza ya juma ni lao na ni "alama" ya mamlaka yake katika mambo ya kidini** (Linganisha Dan. 7:25): ***"Jumapili ilianzishwa na wakatoliki** na unaweza kutetea utakatifu wake kwa misingi ya kikatoliki pekee... Katika Biblia kwanzia Mwanzo hadi Ufunuo, hakuna fungu hata moja linaloidhinisha kubadilishwa kwa Sabato kutoka siku ya saba ya juma hadi siku ya kwanza."* (Catholic Press, Sidney, mnamo tarehe 25-8-1900).



*"Tunaidhinisha Jumapili badala ya Jumamosi kwa sababu kanisa la **katoliki lilitoa utakatifu kutoka Jumamosi hadi Jumapili katika** mkutano wa Laodekia mnamo mwaka wa 364 AD."* ("The Convert's Catechism of Catholic Doctrine" kutoka kwa P. Geiermann, kazi ya Papa Pius wa kumi, tarehe 25-1-1910 aliyepokea Baraka ya mitume).

*"Kanisa la Mungu lilifurahia kubadilisha sherehe kutoka siku ya Sabato hadi siku ya Jumapili."* (Chapisho la katekisimu ya Roma Kurasa wa 247 baada ya uamuzi wa kusanyiko la Trent kwa amri ya Papa Pius wa Tano).

*"Sabato, ambayo ni siku ya saba ya juma ilitunzwa na Kristo na mitume na ilisherehekewa na wakristo wa zama hizo na ilisalia vivyo hivyo hadi ilipobadilishwa katika Mkutano wa Laodekia. Kwanza kabisa, mkutano huu ulijadili swala la siku ya Bwana kisha baadaye wakawazuia watu wasipumzike **katika siku ya saba ya Juma, na kwamba atakayefanya hivyo atalaaniwa.**"* (William Prynne, Mkufunzi maarufu Mwingreza wa mambo ya kidini kutoka kwa kazi yake ya "Dissertation on Lord's Day", ukurasa wa 32).

*"Sabato, siku inayojulikana katika amri, ilibadilishwa na kuitwa siku ya Bwana. Neno hili halijabadilika kwa mujibu wa maneno ya Yesu (Kwa sababu anasema mwenyewe kuwa hakuja kubadilisha sheria, bali kuitimiza) **bali kwa ajili ya mamlaka ya kanisa, sheria hii imebadilika.**"* (Askofu Mkuu wa Rheggio, mahubiri ya tarehe 18-1-1562, Mansi XXIII, ukurasa wa 526).

***"Ni kanisa katoliki lililobadilisha siku ya kupumzika kutoka Jumamosi hadi Jumapili siku ya kwanza ya Juma**... Je, dunia yote inatii mamlaka ya kanisa lipi? Waprotestanti wanadai ya kwamba wanatii Biblia ilhali kwa kuitunza siku ya Jumapili, wanatii sheria ya kanisa Katoliki. **Biblia inasema**, "Ikumbuke siku ya Sabato uitakase", **lakini kanisa katoliki linasema**, "La, uitunze na kuitakasa siku ya kwanza ya Juma" na dunia yote inatii mamlaka ya kikatoliki!"* (Papa Enright tarehe 15-12-1889).

*"Ni dhahiri kuwa **kanisa katoliki** linadai kuwa ni wao waliofanya [kutoka Jumamosi hadi Jumapili] mabadiliko... na kwamba kitendo hicho ni **alama ya mamlaka** yao ya kidini."* (H.F. Thomas, Katibu Mkuu wa Kadinali Gibbons, mnamo tarehe 2-10-1895).

**9.** Katika Ufunuo 13:18, tunapata ishara nyingine, hesabu ya mnyama. *"Yeye aliye na akili, na aihesabu hesabu ya mnyama huyo, maana ni hesabu ya kibinadamu. Na hesabu yake ni mia **sita sitini na sita**."*

Moja wapo wa majina rasmi ya papa ni **"Vicarius Filii Dei"**. Tafsiri yake ni, **"Mwakilishi wa Mwana wa Mungu"**. Katika kuwajibu maswali wasomaji wa jarida la kikatoliki liitwalo "Our Sunday Visitor", la tarehe 18-4-1915, tunasoma: *"Majina yaliopo katika kofia ya Papa ni haya, 'Vicarius Filli Dei'."* Jina hili (ambalo ni makufuru, kwa sababu linajiinua juu ya Roho Mtakatifu (Yoh. 16:12-15, 14:26, Warumi 8:26) ilhali tunafahamu kuwa mwakilishi wa Yesu hapa duniani ni "Roho Mtakatifu") ndilo jina la Mnyama (aya ya 17). Kwa mujibu wa aya ya 17 na 18, tunapata nambari ya jina lake, 666. Katika kilatini baadhi ya herufi zinaweza kuhesabika. Huu ndiyo unabii unaotuonyesha ni nani *"Mpinga Kristo"* (linganisha 2 Wathes. 2:3-12, 1 Yoh. 4:3, 2 Yoh. 7, Warumi 8:3). Katika lugha ya Kigiriki, neno ***"Mpinga Kristo"*** linamaanisha *"mtu ajiwekaye katika nafasi ya Masihi wa Bwana (anti – badala ya, crio - kutiwa mafuta)"*. (Tafsiri halisi ya Agano Jipya, Kurasa ya 371).

Kwa hivyo *"Mpinga Kristo"* ndiye anayedai kuwa mwakilishi wa Kristo – hivi ndivyo anavyodai Papa! Ikiwa Papa angelijitambulisha katika lugha ya agano jipya angalisema hivi: *"Mimi ndimi Mpinga Kristo!"*

| | | |
|---|---|---|
| V* | - | 5 |
| I | - | 1 |
| C | - | 100 |
| A | - | 0 |
| R | - | 0 |
| I | - | 1 |
| U* | - | 5 |
| S | - | 0 |
| F | - | 0 |
| I | - | 1 |
| L | - | 50 |
| I | - | 1 |
| I | - | 1 |
| D | - | 500 |
| E | - | 0 |
| I | - | 1 |
| | | **666** |




***Katika lugha ya kilatini herufi za U Na V ni sawa.**



Yesu Kristo ndiye pekee yake kuhani *"Mkuu wa **kweli katika hekalu** la mbinguni baada ya kupaa mbinguni."* Pia Waeb. 8:1-2. Hapa Kristo hutuonyesha kila siku, jinsi ya kufikia kiti cha neema cha Baba kupitia kwa damu yake (Yoh. 14:6,13,14, War. 8:34) ambaye tunaweza kumwendea wakati wowote kwa njia ya maombi, pasipo kumwendea mtu mwingine yeyote, bali kwa imani na tumaini katika damu ya Kristo (Waeb. 4:14-5:10, 7:25, Math. 6:6-15). Mafundisho kuwa twaweza kumwendea Kristo kupitia mtu fulani au *"kupitia kwa watakatifu waliolala, yanawakilisha makufuru ya mnyama kinyume na Mungu na **hekalu** lake"*, kinyume na upatanisho unaofanyika mbinguni kulingana na Ufunuo 13:6 (na Dan. 8:11-14 na 12:11). Katika mafungu haya hali hii inaelezwa kuwa "uasi juu ya hekalu" au "chukizo la uharibifu".

## ALAMA YA MNYAMA

Siyo alama ya kuonenakana wanayowekewa wanadamu kinyume na mapenzi yao. Ikiwa ungelikataa kukubali alama ya mnyama, basi Mungu kutuonya tusikubali ingekuwa haina maana. Wale wanaokataa *alama ya mnyama* (**ambayo ni ishara ya kumtii au kushikana naye**) wanaelezwa kuwa *"...wale wanaozishika amri za Mungu na kuwa na imani ya Yesu."* Ufunuo 14:12. Ni wale ambao wamepokea mhuri wa Mungu (Ufunuo 7:3,4, 14:1) na wamepata ushindi dhidi ya alama ya mnyama (Ufunuo 15:2, Dan. 3). Alama ya mnyama inahusisha uasi wa amri za Mungu (Yak. 2:10). Kwa sababu mhuri wa Mungu, ishara ya mamlaka yake, tunaipata katika amri kumi (soma chini yake).




Alama ya mnyama itatiwa katika kipaji cha uso au katika mkono (Ufunuo 13:16, 14:9). Kipaji cha uso kinawakilisha kujulishwa (imani, ufahamu). Mkono unawakilisha kitendo (kutunza au kutotunza amri). Jambo hili linaonyeshwa katika Kum. la Torati 11:8,18 (Kum. la Torati 13:1-6) ambapo tunasoma kuhusu kutunza amri *zote* kumi.

**Yeyote anayeelewa majukumu yanayohusu amri ya nne, ambayo Mungu anasema ndiyo ishara ya mamlaka yake, na huku anayakataa mamlaka hayo, na badala yake anaheshimu kile ambacho Rumi imeweka kuwa ishara ya mamlaka yake, yeye amekwisha kubali ishara ya kushikana na Rumi, ambayo ni alama ya mnyama.** Ni wakati ambapo sheria ya kutunza Jumapili itakapowekwa, ndiposa mwanadamu atahitajika kuchagua kati ya amri za Mungu na amri za wanadamu; hapo ndipo wale watakaozidi kudumu katika kuiasi amri watakapopokea alama ya mnyama. Kwa yeyote anayetunza amri ya Jumapili kwa kutokujua, Mungu anasema hivi, *"Nyakati za ujinga Mungu alijifanya haoni, lakini sasa anawaita wote katika toba."* (Matendo 17:30).


## MUHURI WA MUNGU

**Alama au muhuri huonyesha mambo sawa katika Biblia** (Warumi 4:11).

Muhuri rasmi lazima uonyeshe mambo matatu:

1. Jina la mwenye kutoa sheria (Abraham Lincoln)
2. Mamlaka yake (Rais)
3. Eneo lake (Marekani)

Muhuri wa Mungu, ulio ishara ya milele ya agano lake una uhusiano na sheria zake na tunaupata katika amri ya nne (Kut. 20:8-11): *"Ikumbuke siku ya Sabato uitakase, siku sita fanya kazi na utende mabo yako yote. **Lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana Mungu wako;** katika siku hiyo usifanye kazi yoyote, wewe wala mwana wako, wala binti yako, wala mjakazi wako wakike, wala mjakazi wako wa kiume, wala ng'ombe, wala mgeni aliye ndani ya malango yako; **kwa maana katika siku sita Bwana alifanya mbingu na nchi na bahari na vyote vilivyomo, na akapumzika siku ya saba, kwa hiyo Bwana alibariki siku ya saba na kuitakasa.**"* (Pia Kut. 31:13,17-18).




Ingawa amri zote ni sawa mbele za Mungu (Yak. 2:10), tunapata Muhuri wa Mungu katika amri ya nne:

1. Jina la Mungu: ***"Bwana Mungu wako"***
2. Mamlaka: ***"Muumba"***
3. Eneo lake: ***"Mbingu, nchi na bahari na vyote vilivyomo"***

Biblia huongea kuhusu Sabato kama ishara yake ya **milele**: *"...hakika mtazishika sabato zangu, ni ishara kati yangu na ninyi **(milele)**; ili mpate kujua mimi ndimi Mungu niwatakasaye"* (Kut. 31:13, pia 31:16,17, Eze. 20:12,20).

Yesu anasema: *"Msidhani ya kwamba nalikuja kuitangua torati au manabii, la sikuja kutangua bali kutimiza. **Amin, amin nawaambia, hadi mbingu na nchi zitakapopita, yodi moja wala nukta moja havitaondoka hadi yote yatakapotimizwa.**"* (Math. 5:17-18).

Mtu mmoja alikuja na kumwuliza Yesu: ***"Mwalimu mwema, nifanye nini ili niuridhi ufalme wa mbinguni"*** Yesu akajibu, ***"Ukitaka kuingia katika ufalme, shika amri**... usiue, usizini, usiibe, usimshuhudie jirani yako uongo..."* Math. 19:16-19.

Sabato ya siku ya Saba ni moja ya sehemu muhimu ya sheria ya Mungu, **kumbusho la kila juma kuwa Kristo ndiye Muumba na Mwokozi wetu.**

*"Hapo mwanzo kulikuwa na Neno, na Neno alikuwa kwa Mungu na Neno alikuwa Mungu... Vitu vyote viliumbwa na yeye... na Neno akafanyika mwili, akakaa nasi, amejaa neema na kweli."* (Yoh. 1:1-3,14).

Sawa na ahadi waliopewa waisraeli wakati wa kuingia kanani, ndivyo Sabato ilivyo kumbusho la ahadi ya pumziko la Sabato ya kanani ya mbinguni (2 Pet. 3:13, Waebrania 11:10,39-40, Ufunuo 21:2). Pumziko litakalopatikana wakati wa kurudi kwa Yesu (Waeb. 3:10-19, 4:1-11, Kum. la Torati 4:1-2, 1 Wakor. 10:11-13) baada ya kuzunguka dunia hii kwa miaka elfu sita **(6000)** tangu kuanguka kwa mwanadamu.

Ukihesabu miaka ya kila kizazi tangu Adamu utapata ni miaka elfu nne **(4000)** hadi kuzaliwa kwa Yesu (Atlas of World History, 1990 by K. Thienemanns Press, Stuttgart-Vienna). Kisha tunafahamu kuwa tunaelekea **mwisho wa milenia ya sita (6th millennium)** ya mwanadamu jinsi ilivyotabiriwa na Mungu. Kuhusu kurudi kwa Yesu tunasoma: *"...siku moja kwa Bwana ni sawa na miaka elfu, na miaka elfu ni sawa na siku moja"* (2 Petro 3:8). Je, wajua kuwa *"... iko karibu, hata mlangoni"?* Math. 24:33.

**Katika agano jipya, watu wa Mungu wanaitwa *Israeli wa Kiroho*** ambao kwa imani wamepokea tohara ya rohoni (Wakolosai 2:11-12, Warumi 2:28-29, Wagalatia 3:6-9,28-29, 5:6, 6:15, Warumi 11:25, 1 Petro 2:9-10). Agano jipya na Kristo humfanya mtu kiumbe kipya. Nabii Yeremia alitabiri hivi: *"...hili ndilo agano nitakalolifanya na nyumba ya Israeli, baada ya siku hizo asema Bwana, nitaziweka sheria zangu ndani mwao, nao watakuwa watu wangu."* (Yer. 31:31-33).

Kwa hivyo watu wa Mungu daima wataidumisha amri: *"Na joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake akafanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu."* Ufunuo 12:17. (Katika unabii, mwanamke bikira huwakilisha kanisa safi, na mwanamke kahaba huwakilisha kanisa lililoasi - 2 Wakor. 11:2, Eze. 16, Ufunuo 17, 18).

**Sasa tunaelewa ni nini maana ya ujumbe wa malaika watatu katika Ufunuo 14:**

**1.** Malaika hawa hutuambia kuwa **hukumu**, *uamuzi wa umilele wetu* unaendelea huko mbinguni. Ufunuo 14:6-7.




**2.** Hutuambia kuwa uprotestanti **pia** ulianguka (verse 8) na pia Ufunuo 18:1-5 *"...umekuwa maskani ya mashetani na ngome ya kila pepo mchafu."* Kwa kila mkristo (watu wake) halisi, malaika anatusihi: ***"...tokeni kwake enyi watu wangu msishiriki dhambi zake wala kupokea mapigo yake"*** Ufunuo 18:4.

**3. Hii ni onyo kali na ya upendo kutoka kwa Mungu kuelekea dunia yote:** Wote watakaosujudia upapa au sanamu ya uprotestanti au sanamu ya muungano wa makanisa yalioasi, watakapokubali kutii sheria ya Jumapili ilhali wakijua wenyewe kwamba kufanya hivyo ni makosa, wataipokea alama ya mnyama na baadaye kifo cha milele (Ufunuo 14:9-11).


**4.** Katika Ufunuo 14:12, tunapata kikundi cha watu wasioipokea alama ya mnyama. Wanatunza sheria **yote** ya Mungu, ikiwemo amri ya sabato ya siku ya saba (Matendo 7:38) na imani ya Yesu.

## Je, utasimama siku ya hukumu?

Malaika wa kwanza anaongea kuhusu hukumu itakayofanyika mbinguni **kabla** ya kurudi kwa Yesu (Dan. 7:9-12, 2 Wakor. 5:10). Kwa sababu hukumu lazima ifanyike kabla ya kufufuliwa kwa yule atakayeridhi ufalme, na yule atakayekuwa hai wakati wa kurudi kwake Mwokozi (1 Wathes. 4:15-17, Yoh. 5:27-29, Ufu. 20:5-6). Zaidi ya hayo, Biblia huongea kuhusu hukumu itakayofanyika mbinguni miaka elfu moja (1000) **baada** ya kurudi kwake Kristo ambapo wale walio waaminifu watashiriki katika kuwahukumu wafu wasioamini na malaika walioasi (Dan. 7:22, 1 Wakor. 6:2-3, Ufu. 20:4). Hukumu hii itapitishwa na kutangazwa **baada** ya miaka elfu moja (1000) katika ufufuo wa wasioamini (Yoh. 5:29, Ufu. 20:7-15). Amri kumi ndicho kipimo kisichobadilika katika siku ya hukumu ya Mungu (Muhubiri 12:13-14, Ufu. 11:18-19, Zab. 89:34, Math.7:21). Jambo hili ni dhahiri katika mfano wa kipekee wa Yesu (Wafilipi 2:5, Warumi 15:5), inayosema *"Ninafurahi kuyatenda mapenzi yako ee Bwana, naam, sheria yako imo moyoni mwangu."* (Zab. 40:8, pia Yoh. 6:38, 4:34, Zab. 40:7-9, Waebrania 10:9, Lk. 22:42). Katika sala ya Bwana tunasoma *"mapenzi yako yatendeke"*, lakini je, mapenzi ya Mungu yanaweza kufanyika katika maisha yetu ya dhambi? Biblia husema *"dhambi ni uasi wa sheria"* 1 Yoh. 3:4, pia *"mshaara wa dhambi ni mauti"* Warumi 6:23. Kisha kutoka kinywani mwa nabii tunaulizwa: *"Je! Mkushi anaweza kuibadili ngozi yake, au chui madoadoa yake? Kama aweza ndivyo ninyi mwaweza kutenda mema, ninyi mliozoea kutenda mabaya."* Yer. 13:23, Warumi 7:24. Tukijiangalia maisha yetu, tunaelewa ya kuwa sisi kivyetu, kwa nguvu zetu wenyewe, hatuwezi kuepuka hukumu ya Mungu na mauti yake. Lakini Mungu ametutengenezea **njia ya wokovu** sisi sote tuliokuwa mateka wa shetani.



Njia hii, iliyotengenezwa na upendo wa Mungu inaitwa **"Yesu Kristo"**. *"Kwa maana jinsi hii Mungu alupenda ulimwengu, akamtoa mwana wake wa pekee ili kila amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele."* Yoh. 3:16. Golgotha ni ukumbusho wa kujitolea kwake, ambako kulikuwa ni kwa lazima kwa ajili ya kuiasi amri ya Mungu. Kwa hivyo hatustahili kuiona dhambi kama kitu kisichoweza kutudhuru. Warumi 6:15,n.k. Huruma za Mungu juu yetu siyo huruma ya bei rahisi. Inatubidi kujitolea kwa Mungu na kujinyima. Yesu anasema: *"Mimi ndimi njia, kweli na uzima, hakuna mtu ajaye kwa Baba isipokuwa kwa mimi."* Yoh. 14:6. Kupitia kwa maisha yake, Yesu ametuonyesha njia ya kumfikia Baba, na njia ya uzima wa milele.



## KUPONI

Uliza vitabu vifuatavyo bila malipo.

☐ **BIBLIA**
Bure!

☐ **THE GREAT CONTROVERSY (Vita Kuu)**
Kitabu hiki kimechapishwa katika lugha arobaini tofauti tofauti, kinatueleza jinsi Biblia inatufundisha kuhusu wakati uliopita, uliopo na ujao. Bure!

☐ **STEPS TO CHRIST (Njia Salama)**
Kitabu hiki kinatuonyesha hatua kwa hatua jinsi ya kumfikia Kristo. Bure!

Jina lako: ______________________

Anwani: ______________________

______________________

______________________


Kisha tuma kwa:


**The Fiwagoh Mission Orphanage Ministries**
**S. L. P. 14390**
**Nakuru-20100**
**Kenya. E. Africa**
**Barua Pepe: fiwagohmi@yahoo.com**
**Simu: 0720-224-465 or 0711-733-834**



Bila malipo au majukumu!


**Tunawezaje kuupokea uzima wa milele katika Kristo?**
Jibu la Yesu leo ni lile lile alilolitoa pale mwanzo: *"...shika amri...na unifwate!"* Math. 19:17,21, 1 Petro 2:21-25, Ufunuo 14:4.

Kumfuata Kristo hivi leo, maana yake ni kujifunza kuhusu maisha ya Yesu jinzi ilivyoandikwa katika Biblia (Yoh. 5:39, 8:31-32, 3:36, Waeb. 5:8-9, 11:8,n.k., Yak. 4:7, Warumi 16:26). Roho Mtakatifu atakuwa na mvuto juu yetu kama siku ya pentekoste, wakati watu walipokiri dhambi zao na kuuliza: *"Nasi tufanye nini?"* Petro akajibu: *"Tubuni!"* Matendo 2:37-38. Na wakati mwingine akasema: *"Tubuni basi mrejee, ili dhambi zenu zifutwe."* Matendo 3:19.




Amri ya Mungu kama kioo, hutuonyesha uchafu na dhambi zetu (Warumi 4:15, 3:20, 7:7), ambazo Yesu anataka kuzifuta kupitia kwa damu yake. Huu ndio mwanzo wa upendo wa binadamu kwa Mungu. Yesu akiongea kuhusu yule mwanamke mwenye dhambi, alisema: *"Amesamehewa dhambi zake ambazo ni nyingi, kwa kuwa amependa sana..."* Lk. 7:47. *"Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza... maana huku ndiko kumpenda Mungu* (majibu yetu) *kwamba tuzishike amri zake, wala amri zake si nzito"* 1 Yoh. 4:19, 5:3. Katika kumpenda Yesu tunapokea nguvu za kushinda dhambi kutoka kwa Mungu. *"Mkinipenda, mtazishika amri zangu...Nami nitamwomba Baba, Naye atawapa msaidizi mwingine...ndiye Roho wa kweli."* Yoh. 14:15-17. Upendo na nguvu za Roho Mtakatifu tunazozipokea hutuwezesha kushinda dhambi jinsi ambavyo Kristo alivyoshinda. Yoh. 15:10, 1 Yoh. 5:4-5, Ufunuo 3:21.





Yesu Kristo, kwa kuuchukua mwili wa binadamu (Wafil. 2:5-8, Yoh. 16:28) tumehakikishiwa kuwa Mungu anajua ni nguvu za aina gani tunazozihitaji ili kuyatekeleza mapenzi yake na kutuwezesha kustahimili majaribu ya kibinadamu. *"Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti, yaani Ibilisi awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti, walikuwa katika hali ya utumwa, maana ni hakika, hatwai asili ya malaika, ila atwaa asili ya mzao wa Ibrahimu. Hivyo ilimpasa kufananishwa na ndugu zake katika mambo yote, apate kuwa Kuhani Mkuu mwenye rehema, mwaminifu katika mambo ya Mungu, ili afanye suluhu kwa dhambi za watu wake."* Waebrania 2:14-18.



Tunaweza kuzipokea nguvu hizi za kushinda dhambi mradi tu tunaamini katika haki ya Kristo iliyo ya kipekee (maisha yasyio ya dhambi - linganisha Warumi 8:3, Waeb. 4:15), na pia mtu binafsi akubali kwa imani kujitolea kwa Yesu kuwa kafara. Yoh. 6:28-29, 3:16, 1:29.

## M W A L I K O !

Ukihisi kwamba ungependa kushiriki na mojawapo wa makanisa yetu hapa nchini, tuandikie, utupe anwani na nambari yako ya simu. Tutafurahi kukushikanisha na mojawapo wa makanisa yetu nchini.

Tupashe habari kwa kutuandikia barua au kupiga simu: 0726-394-046 / 0720-224-465.

Barua pepe: fiwagohmi@yahoo.com


**The Fiwagoh Mission Orphanage Ministries**

**S. L. P. 14390**

**Nakuru–20100**

**Kenya. E. Africa.**


Yesu hakufa kwa ajili ya dhambi zake. Tunasoma hivi: *"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye."* 2 Wakor. 5:21 (1 Yoh. 3:5, Yoh. 8:46). Maana yake kuwa tutubu na kuwacha haki yetu, tukiri na kuwacha dhambi (Kuasi amri ya Mungu) na kisha tumtii (Meth. 28:13, 1 Yoh. 1:6-10, 2:4, 3:3-10, 1 Petro 2:21, Math. 10:34-39).

Imani na toba ni vipawa vya Mungu kwa wale wanaomtafuta kwa moyo mnyofu. Mungu atatenda kazi pamoja na sisi kupitia kwa Roho Mtakatifu ikiwa tutampa nafasi. Imani huja kwa kulisoma na kulitangaza neno la Mungu. Warumi 10:17. Yesu alisema: *"Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mnao uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia"* Yoh. 5:39 (Lk. 24:25-27, Yoh. 2:22, Warumi 16:26, Matendo 17:11,12).




Kuuchunguza unabii uliotimizwa kikamilifu (Unaohusu historia ya dunia na kurudi kwake Mwana wa Adamu), utaimarisha imani yetu katika mpango wa ukombozi kupitia kwa Yesu Kristo na kuweka msingi imara wa imani yetu (2 Petro 1:19-21). Ili tuimarike katika kulisoma neno la Mungu tumeahidiwa mwalimu wa kutoka juu. *"Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha wote na kuwakumbusha yote niliyowaambia, ...atawaongoza awatie kwenye kweli yote ...neno lako ndiyo kweli."* Yoh. 14:26, 16:13, 17:17. Yeyote anayekataa mwaliko wa huruma za Mungu, hukataa kulisikiliza neno la kweli, wala halisomi, wala kulijaribu, hatapokea nguvu ziokoazo kwa imani za Mungu, mwishowe atakuwa miongoni mwa wale wa kuangamia milele. Jer. 6:17-19, 9:12-15, Hos. 4:6.

*"Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu,wala hakemei; naye atapewa."* Yak. 1:5. Yesu anatuambia: *"Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa ...basi ikiwa ninyi, mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, Je! Si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wao wamwombao?"* Math. 7:7,11. Basi, kama Daudi tuulize: *"Ee Mungu, uniumbie moyo safi."* Zab. 51:10 (Zab. 139:23-24).

Yeyote atakayeamini na kuomba kwa uaminifu atapata ujuzi: *"Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu."* Wafilipi 4:13.

Kadri tunavyomfuata Kristo kwa moyo mnyoofu, na kumtumainia kama mkombozi wetu aishiye, ndivyo tutakavyo kuza tabia njema kama yake na kuwa tayari kumlaki ajavyo. *"Hili ni agano nitakaloagana nao baada ya siku zile, anena Bwana, nitatia sheria zangu mioyoni mwao, na katika nia zao nitaziandika."* Waeb. 10:16 (Yer. 31:33).



Unakumbuka kwamba uaminifu wa mwanadamu ulijaribiwa na tunda pale Edeni (mti wa kujua mema na mabaya - Mwanzo 2:16-17)? Vivyo hivyo, siku za mwisho mwanadamu atajaribiwa na amri spesheli ya Mungu. Yak. 2:10. Joka mdanganyifu akasema: *"Hivyo ndivyo alivyosema Mungu?"*



Ni hasara kiasi gani aliyoipata mwanadamu kwa kutotii?! (Mwanzo 3). Shaka kulihusu neno la Mungu tayari linapandwa mioyoni mwa watu na yule adui kwa kusema: *"Mungu anamaanisha hivyo kuhusu sabato ya siku ya Saba?"*

Watu watakapofahamu kuwa Jumapili ni amri ya mwanadamu, itawabidi kuyakumbuka maneno ya Yesu: *"Akawaambia, Isaya alitabiri vema juu yenu ninyi wanafiki, kama ilivyandikwa, watu hawa huniheshimu kwa midomo, ila mioyo yao iko mbali nami ...wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu ...mwaikataa amri ya Mungu mpate kuyashika mapokeo yenu."* Marko 7:6-9.

Mungu anawaonya watu wake kupitia nabii Ezekieli: *"...msiende katika amri za baba zenu, wala msizishike hukumu zao* [mila], *wala msijitie unajisi kwa vinyago vyao. Mmi ni Bwana Mungu wenu; endeni katika amri zangu, mkazishike hukumu zangu, na kuzitenda;* ***zitakaseni sabato zangu****, zitakuwa* ***ishara*** *kati ya mimi na ninyi, mpate kujua ya kuwa mimi ndimi BWANA, Mungu wenu."* Ez. 20:18-20, Yer. 9:12-13.

Maagizo na itikadi za wanadamu haziwezi kutuweka huru na msingi wa ukristo usemao: *"Imetubidi kumtii Mungu kuliko wanadamu."* Matendo 5:29, 4:19.

**Uamuzi wako ni nini - sabato ya Bwana, au Jumapili ya Upapa?** (Yer. 10:2, 1 Wafalme 18:21, 1 Sam. 15:22,23).


**Muhuri wa Mungu**




Roho Mtakatifu anatuonya: *"Leo, kama ilivyonenwa tangu zamani, leo kama mtasikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu... kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake. Basi, na tufanye bidii kuingia katika raha* (sabato-) *ile, ili kwamba mtu yeyote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi."* Waeb. 4:7,10-11.

Wale watakaookolewa ni wale Biblia inaowataja kuwa: *"Hapa ndipo penye subira, hawa ndio wazishikao amri za Mungu na kuwa na imani ya Yesu."* Ufunuo 14:12.

**Alama ya mnyama**




Mapigo na hukumu za Mungu hivi karibuni zitawaangukia wale walio na alama, jina au nambari ya mnyama, au atayeabudu mnyama na sanamu yake (watakaotii mpinga Kristo, mamlaka ya dini iliyoshirikiana na serikali) na wale kwa matendo yao, wameyakataa mashauri na maonyo ya Mungu (Ufunuo 13:16-18, 14:9-11, 16:2, 18, 19:19-21).

Ujumbe huu wa saa ya hukumu unaweza kusababisha hofu ndani ya watu wengine. Lakini hakika ni kwamba, ujumbe huu ni kwa ajili ya wokovu wetu, ujumbe kutoka kwa Mungu mwenye upendo, *"maana hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikilie toba."* 2 Pet. 3:9.

Yeyote aliye mwaminifu atatambua ya kwamba: *"Kumcha Bwana ndio chanzo cha hekima."* Meth. 1:7, Lk. 12:4-5, Kut. 20:20. Chanzo cha hofu au kuogopa ni dhambi. Mwanzo 3:10,11. Lakini tukikubali msamaha kupitia upendo wa Mungu katika Kristo, tutafahamu kwamba: *"Katika pendo, hamna hofu... na mwenye hofu hakukamilishwa katika pendo. Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza."* 1 Yoh. 4:18-19.

Hofu ya kupotea inabadilishwa na kuwa tumaini la wokovu, na badala ya kumwogopa Mungu, unamheshimu na kumpenda. Kukosa tumaini kunaondoka na badala ya hofu, ni tumaini la furaha la kutimizwa kwa ahadi za Mungu. Toleo la Mungu, mda wa kutubu na kurejea, ni wa kitambo kidogo tu! Tumia wakati huu kwa kujihoji wewe mwenyewe na urejee kwa sababu mda wa rehema ni mfupi na baadaye Yesu arejee. Ishara za nyakati zinatuonyesha kwamba tunaishi katika nyakati za mwisho wa **historia ya ulimwengu huu!**

***"Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwizi; katika siku hiyo mbingu zitatolewa kwa mshindo mkuu, na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea... kwa hiyo, wapenzi, kwa kuwa mnatazamia mambo hayo, fanyeni bidii ili mwonekane katika amani kuwa hamna mawaa wala aibu mbele yake."*** 2 Petro 3:10,14, Isaya 55:6-9, Mal. 3:17,18, 4:1-2.



***"Hii ndiyo jumla ya maneno:*** *yote yamekwisha sikiwa; mcheni mungu, na kuzishika amri zake, maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu. Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, ikiwa jema au likiwa baya."* Muhubiri 12:13-14.

